OFISI YA RAIS

# UTUMISHI

NA UTAWALA BORA




Toleo la
Oktoba - Desemba, 2025

# YALIYOMO


| | | |
|---|---|---|
| 1 | UAPISHO WA WAZIRI NA NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA | 1 |
| 2 | MHE. KIKWETE ATOA WITO KWA WATUMISHI WA UMMA KUONGEZA KASI YA UWAJIBIKAJI ILI KUTOA HUDUMA BORA KWA WANANCHI | 2 |
| 3 | SERIKALI KUJENGA UTUMISHI WA UMMA WENYE UFANISI, UWAJIBIKAJI NA KUONGEZA FURSA ZA AJIRA NA USTAWI WA VIJANA | 4 |
| 4 | MHE. RIDHIWANI KIKWETE AWAKUMBUSHA SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA KUZINGATIA WAJIBU WAO WA KUSIMAMIA MAADILI BILA UPENDELEO | 6 |
| 5 | MHE. QWARAY ATOA WITO KWA VIONGOZI KUENDELEA KUJIFUNZA ILI KUBUNI MIKAKATI YA KUBORESHA UTENDAJI | 8 |
| 6 | FAHAMU KUHUSU GAZETI LA SERIKALI | 11 |
| 7 | SERIKALI YATOA VIBALI VYA AJIRA 86,500 KATIKA MWAKA WA FEDHA 2024/25 NA 2025/26 | 14 |
| 8 | WATUMISHI WA UMMA WAKUMBUSHWA KUZINGATIA MAADILI KATIKA UTENDAJI KAZI ILI KUTOA HUDUMA BORA KWA WANANCHI | 16 |
| 9 | "IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA NI KIUNGO MUHIMU KATIKA HISTORIA YA NCHI YETU"- MHE. RIDHIWANI KIKWETE | 19 |
| 10 | MATUKIO KATIKA PICHA YAKIONYESHA USHIRIKI WA OFISI YA RAIS-UTUMISHI NA UTAWALA BORA KATIKA WIKI YA HUDUMA KWA MTEJA KUANZIA TAREHE 6-10 OKTOBA, 2025 ILIYOKUWA NA KAULIMBIU ISEMAYO DHAMIRA INAYOWEZEKANA. | 21 |
| 11 | KATIBU MKUU MKOMI AWASISITIZA WATUMISHI WA UMMA KUDUMISHA AMANI | 22 |
| 12 | WITO WATOLEWA KWA WATUMISHI WA UMMA KUBADILIKA KIMTAZAMO KATIKA UTENDAJI ILI KUFIKIA MALENGO YA DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2050 | 24 |
| 13 | MRADI WA UJENZI WA MAKAZI YA WATUMISHI WA UMMA SEKTA YA ELIMU NA AFYA KUONGEZA TIJA KATIKA UTENDAJI KAZI | 27 |
| 14 | TUJIKITE KUFUNDISHA KOZI ZITAKAZOENDA KUTATUA CHANGAMOTO ZA WAHITIMU NA WANANCHI - MHE. KIKWETE | 28 |
| 15 | MHE. RIDHIWANI KIKWETE AITAKA SEKRETARIETI YA AJIRA KUHARAKISHA NA KUWEKA WAZI MCHAKATO WA AJIRA 12,000 ZILIZOTANGAZWA NA RAIS MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN | 30 |
| 16 | HABARI KATIKA PICHA | 32 |

# 1 UAPISHO WA WAZIRI NA NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akimuapisha Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwenye hafla fupi iliyofanyika Ikulu Chamwino-Dodoma tarehe 18 Novemba, 2025.*




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akimuapisha Mhe. Regina Ndege Qwaray kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwenye hafla fupi iliyofanyika Ikulu Chamwino-Dodoma tarehe 18 Novemba, 2025.*

# MHE. KIKWETE ATOA WITO KWA WATUMISHI WA UMMA KUONGEZA KASI YA UWAJIBIKAJI ILI KUTOA HUDUMA BORA KWA WANANCHI

*Na Mwandishi Wetu - Dodoma*

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwani Kikwete amewataka watumishi wa Ofisi hiyo kuwa tayari kufanya kazi kwa kasi na kutoa huduma bora kwa wananchi.

"Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati wa kampeni aliahidi mambo mengi na anatamani matokeo yaonekane kwa wananchi ndani ya muda mfupi, hivyo tunatakiwa kuongeza kasi na kukamilisha ahadi zake kwa wakati" alisema Mhe. Kikwete.

Waziri Kikwete aliyasema hayo alipokuwa akiongea na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais-UTUMISHI na Menejimenti ya Ofisi hiyo Novemba 18, 2025 wakati wa makabidhiano ya Ofisi hiyo Mtumba Jijini Dodoma.

Mhe. Ridhiwani amesema Serikali inaendelea kuboresha Utumishi wa Umma ili kumkomboa mwananchi na changamoto ya upatikanaji wa huduma bora.

Pia, Mhe. Kikwete amesema anatambua uhitaji mkubwa wa Watanzania hasa kwenye suala la ajira na kuelezea mkakati mkubwa utakaofanywa na Serikali katika kutatua changamoto ya ajira kwa Watanzania.

Kwa upande wake Naibu Waziri Mhe. Regina Qwaray amewasisitiza watumishi wa Ofisi hiyo kutoa ushirikiano kwa viongozi na watumishi wengine katika utendaji huku kila mmoja akitambua nafasi na thamani ya mwingine ili kufikia malengo ya Serikali ya utoaji wa huduma bora kwa ustawi wa taifa.rasilimaliwatu na vitendea kazi ni utashi alionao kwa TAKUKURU ili iweze kufanya kazi yake kwa ufanisi.



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete (wa tatu kulia) akikabidhiwa Nyaraka za Ofisi na aliyekuwa Waziri wa Ofisi hiyo, Mh. Boniface Simbachawene (wa pili kulia) wakati wa makabidhiano ya ofisi yaliyofanyika tarehe 18 Novemba, 2025 Jijini Dodoma.*



*Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Bw. Juma Mkomi (aliyesimama) akitoa neno la utangulizi wakati wa makabidhiano ya Viongozi wateule wa ofisi hiyo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete na Naibu Waziri wa ofisi hiyo Mhe. Regina Qwaray yaliyofanyika tarehe 18 Novemba, 2025 Jijini Dodoma.*



*Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Bw. Xavier Daudi (aliyevaa miwani) akimsikiliza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Ridhiwani Kikwete (hayupo pichani) alipokuwa akizungumza na Menejimenti na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi hiyo baada ya Waziri huyo kukabidhiwa Ofisi tarehe 18 Novemba, 2025 Jijini Dodoma.*



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete (wa pili kutoka kushoto mstari wa kwanza) akiwa katika picha ya pamoja na Wakurugenzi wa Idara na Vitengo mara baada ya kuwasili katika ofisi hiyo iliyopo Mtumba jijini Dodoma.*

# 3 SERIKALI KUJENGA UTUMISHI WA UMMA WENYE UFANISI, UWAJIBIKAJI NA KUONGEZA FURSA ZA AJIRA NA USTAWI WA VIJANA

*Na Veonica Mwafisi - Dar es Salaam*

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete amesema Serikali kupitia Ofisi yake inaonesha dhamira thabiti ya kujenga Utumishi wa Umma wenye ufanisi, uwajibikaji na unaozingatia misingi ya utawala bora ili kwenda sambamba na matarajio ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050.

Waziri Kikwete amesema hayo wakati wa Mkutano wake na Waandishi wa Habari uliofanyika katika Ukumbi wa Habari Maelezo jijini Dar es salaam Desemba 12, 2025. Mkutano huo ulilenga kutoa taarifa ya namna Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inavyotekeleza wajibu wake kwa Taasisi za umma, Watumishi wa Umma na Wananchi kwa jumla.

Mhe. Kikwete ameongeza kuwa, dhamira hiyo imeweka vipaumbele ambavyo ni kuongeza fursa za ajira na ustawi wa vijana wa kitanzania, maboresho ya mifumo ya ajira, utoaji wa huduma, mafunzo ya kujenga uwezo, usimamizi wa rasilimaliwatu pamoja na kuimarisha mifumo ya mawasiliano kati ya Serikali na wananchi.

Mhe. Kikwete alibainisha kuwa Serikali inaendelea kuhakikisha nafasi za ajira katika Utumishi wa Umma zinakuwa za wazi na ushindani kupitia Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (PSRS) ili kuwajengea Watanzania imani na uaminifu kwa Serikali yao kwa ustawi wa Taifa.

Vile vile, Mhe. Kikwete amesema, kupitia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 imeelekeza Sekta ya kipaumbele iwe na uwezo wa kuzalisha ajira na kuongeza fursa ya ajira kwa vijana, kuongeza kipato kwa wananchi na kupunguza umaskini kwa kuzingatia viwango vya juu vya weledi unaopatikana na kufuata misingi ya haki, umahiri na utendaji bora.

Aidha, Mhe. Kikwete ameongeza kuwa, katika kufanikisha maelekezo ya Dira 2050, kupitia Serikali kwa mwaka wa Fedha 2025/26 kibali cha nafasi 41,500 za ajira zikiwemo nafasi 12,000 za ajira ambazo ni ahadi ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoahidi kutoa nafasi 5,000 za kada za Afya na nafasi 7,000 za Walimu wa Masomo ya Sayansi na Hisabati ambazo ni uzalishaji wa ajira zilizo rasmi ndani ya siku 100 baada ya kuingia madarakani.

Mhe. Kikwete amesema kuwa, ili kuhakikisha usaili unafanyika kwa wakati na kwa lengo la kuongeza ufanisi, usaili wa mchujo wa nafasi hizo utafanyika kwa kutumia mfumo wa kieletroniki uitwao “Online Aptitude Test (OATS)” na utafanyika katika vituo mbalimbali kama vile Taasisi za Elimu ya Juu, Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi na Ufundi Stadi (VETA) na Shule za Sekondari zenye maabara za Komputa zinazopatikana katika mikoa yote na Vituo mahsusi kwa Unguja na Pemba.

“Mhe. Rais Dkt. Samia aliahidi baada ya kuingia madarakani atatoa nafasi 5,000 za kada za Afya na nafasi 7,000 za Walimu ndani ya siku 100 na tayari nafasi za ajira 12,000 zimeshatangazwa na waombaji wenye sifa wameitwa kwenye usaili utakaofanyika kuanzia tarehe 13 Desemba, 2025 katika mikoa yote Tanzania Bara na Vituo mahsusi kwa Unguja na Pemba,” Amefafanua Mhe. Kikwete.

Pia, Waziri huyo aliwaomba wandishi wa habari kuendelea kuwahabarisha na kuwaelimisha Watanzania hususan vijana, kutambua fursa zilizopo na kuzitumia kwa manufaa ya taifa. Utambuzi huo unaifanya Serikali kuendelea na jitihada zake za kukuza ujuzi, kuhimiza maadili, kupanua fursa za makazi bora na kuandaa vijana wa Kitanzania ili kukabiliana na uchumi wa kidijiti.




*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete akizungumza na Waandishi wa Habari (hawapo pichani) wakati wa Mkutano wake na Waandishi hao uliofanyika katika Ukumbi wa Habari Maelezo jijini Dar es salaam uliolenga kutoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi yake.*

*Sehemu ya Waandishi wa Habari wakimsikiliza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete (hayupo pichani) wakati akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo kwenye Mkutano wake na Waandishi hao uliofanyika katika Ukumbi wa Habari Maelezo jijini Dar es salaam. Wa kwanza kulia waliokaa ni Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Regina Qwaray. Wengine ni Viongozi na Watendaji wa Ofisi hiyo.*





*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete (kulia) akiteta jambo na Naibu Waziri wa Ofisi yake Mhe. Regina Qwaray (kushoto) kabla ya kuanza kwa Mkutano wa Waziri huyo na Waandishi wa Habari uliofanyika katika Ukumbi wa Habari Maelezo jijini Dar es salaam kwa lengo la kutoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi yake.*

# 4 MHE. RIDHIWANI KIKWETE AWAKUMBUSHA SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA KUZINGATIA WAJIBU WAO WA KUSIMAMIA MAADILI BILA UPENDELEO



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt.Mwigulu Nchemba (kulia) akiteta jambo na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete (kushoto) baada ya kuwasili katika Ofisi ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ambapo alikuwa na ziara ya kikazi Desemba 11, 2025.*

*Na Antonia Mbwambo na Eric Amani - Dodoma*

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-UTUMISHI na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete, ametoa wito kwa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kuhakikisha inatekeleza majukumu yake kwa weledi, uadilifu na bila upendeleo kwa kiongozi yeyote.

Akizungumza wakati akimkaribisha Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Mwigulu Nchemba kwa ajili ya kuzungumza na watendaji wa Sekretarieti hiyo, Mhe. Kikwete amesisitiza umuhimu wa chombo hicho katika kusimamia maadili kwa kuzingatia misingi ya sheria, uwazi, ukweli na usawa, ili kuendelea kujenga taswira njema ya utumishi wa umma nchini.

Ameeleza kuwa viongozi wa umma wana wajibu mkubwa kwa jamii, hivyo ni muhimu Sekretarieti hiyo kutekeleza dhima yake ya kisheria ya kuhakikisha viongozi wote wanazingatia miiko na maadili katika kutekeleza majukumu yao.

“Hatuwezi kuwa na Serikali ambayo viongozi wanalalamikiwa kwamba ni wapotofu wa Maadili na sisi kama chombo cha kusimamia Maadili ya Viongozi wa Umma tumekaa kimya” Waziri Kikwete alisema.

Aidha, ametoa rai kwa Watumishi wa Sekretarieti ya Maadili kuimarisha ushirikiano, kuendesha uchunguzi kwa haki bila upendeleo na kutoa elimu ya kutosha kuhusu maadili kwa viongozi wa umma na wananchi kwa ujumla.

Kwa upande wao, watendaji wa Sekretarieti hiyo wamemhakikishia Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Mhe. Ridhiwani Kikwete kuwa wataendelea kufanya kazi kwa kuzingatia uwajibikaji, uadilifu na weledi ili kuimarisha imani ya wananchi katika mifumo ya utawala bora.



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete (kushoto) akiteta jambo na Kamishna wa Maadili,Jaji Mstaafu, Bw. Sivangilwa Mwangesi (katikati) wakati wakimsubiria Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba kuwasili katika Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa ziara ya kikazi iliyofanyika Disemba 11, 2025 jijini Dodoma. Wa kwanza kulia ni Katibu Mkuu Ikulu, Bw. Mululi Mahendeka.*



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Mwigulu Nchemba (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi mbalimbali pamoja na menejimenti na watumishi wa Sekretariati ya Maadili ya Viongozi wa Umma wakati wa ziara yake ya kikazi aliyoifanya katika Ofisi hiyo Desemba 11, 2025 Jijini Dodoma. Kulia kwake ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-UTUMISHI na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete na Kushoto ni Katibu Mtendaji Mkuu wa Tume ya Sekretarieti ya Maadili Jaji Sivangilwa Mwangesi.*

# 5 MHE. QWARAY ATOA WITO KWA VIONGOZI KUENDELEA KUJIFUNZA ILI KUBUNI MIKAKATI YA KUBORESHA UTENDAJI




*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Regina Qwaray akizungumza na Viongozi Chipukizi wakati wa uzinduzi wa Programu ya Mafunzo kwa Viongozi hao Awamu ya Kwanza yaliofanyika jijini Dar es Salaam.*

*Na Veonica Mwafisi - Dar es Salaam*

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Regina Qwaray ametoa wito kwa Viongozi kuendelea kujifunza siku kwa siku ili kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia na kitamaduni yatakayowezesha kubuni mikakati mbalimbali ya kuboresha utendaji kwa ustawi wa taifa.

Mhe. Qwaray ameyasema hayo tarehe 11 Disemba, 2025 jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na Viongozi Chipukizi kabla ya kuzindua Programu ya Viongozi hao.

Amesema ili mtu aweze kuwa kiongozi mzuri, ni lazima aendelee kujifunza kila siku kwa lengo la kuweza kukabiliana na changamoto za kiuongozi ikiwemo kubuni mbinu mbalimbali za kusimamia mabadiliko ya kimfumo, kiutawala, kiuchumi, kiteknolojia na kitamaduni yanayojitokeza kila siku.

Mhe. Qwaray amewashukuru na kuwapongeza washirika kutoka Finland na HAUS kwa kukubali kushirikiana na Taasisi ya UONGOZI kubuni na kuandaa programu hii maalumu kwa viongozi na taifa kwa ujumla kwani ina umuhimu wa pekee katika kuendeleza viongozi nchini Tanzania na Afrika kwa ujumla.

Aidha, amewasisitiza Viongozi kushirikiana na watumishi walio chini yao kwa kuwaelekeza kazi badala ya kuwaacha na kuwaona ni tatizo katika utekelezaji wa majukumu yao.

"Kiongozi usiwe mchoyo kufundisha walio chini yako, tuwafundishe, tunakua, tutengeneze viongozi wa baadae, tusishikilie madaraka, tutengeneze viongozi wengi kadri tuwezavyo, Kiongozi hutakiwi kushikilia kila kitu, shirikisha wenzio ili upate mawazo mapya, kuboresha utendaji na kufikia malengo mahususi yaliyowekwa kwa ustawi wa taifa," Mhe. Qwaray amesisitiza.

Amesema Tanzania inaendelea kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs 2030), Ajenda ya Maendeleo ya Afrika (Agenda 2063) na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 na malengo hayo yameweka bayana kuwa mabadiliko ya kiuongozi ni muhimu kwani ndiyo nguzo kuu ya kufikia malengo yaliyowekwa huku akitolea mfano Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 kuwa imeweka malengo ya kuwa na uchumi wa dola trilioni moja ifikapo mwaka 2050.

“Ni dhahiri hatuwezi kufikia lengo hili kama tusipojipanga na kuweka mikakati madhubuti ya kutuwezesha kufikia malengo yetu.”

Ametaja moja ya mikakati hiyo ni pamoja na kuwa na nguvu kazi yenye uwezo na motisha pamoja na kuwajengea uwezo viongozi kupitia mafunzo kama haya.

Programu hii ni muhimu sana kwani itasaidia Serikali kuwa na viongozi watakaotimiza matarajio ya wananchi. “Nina imani kuwa maarifa na ujuzi utakaotolewa kwa washiriki wa programu hii utawapa msingi bora na utayari kuongoza na kutoa huduma bora kwa wanachi.

Mhe. Qwaray amewashauri viongozi kujifanyia tathmini ili kutambua uwezo na udhaifu wao kwani kwa kufanya hivyo itasaidia kuboresha utendaji hasa kwenye eneo la mapungufu.

Akitoa neno la utangulizi kabla ya kumkaribisha Naibu Waziri kuzindua Programu hiyo, Afisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya UONGOZI, Bw. Kadari Singo amesema Taasisi yao imekuwa ikitoa mafunzo mbalimbali ya uongozi ili kuwa na viongozi bora katika taifa.

“Kunaweza kukawa na mifumo mizuri lakini viongozi sio wazuri, hivyo mafunzo tunayoyatoa yanasaidia kuwajenga viongozi kuendana na mifumo mizuri iliyopo,” Bw. Kadari ameongeza.




*Sehemu ya Viongozi Chipukizi wakifuatilia hotuba ya Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Regina Qwaray (hayupo pichani) wakati akizindua Programu ya Mafunzo kwa Viongozi hao Awamu ya Kwanza yaliofanyika jijini Dar es Salaam.*




*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Regina Qwaray (wapili kutoka kulia) akiwa katika uzinduzi wa Programu ya Mafunzo kwa Viongozi Chipukizi Awamu ya Kwanza yaliofanyika jijini Dar es Salaam. Kulia kwake ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya UONGOZI, Bw. Kadari Singo. Wengine ni Watendaji wa taasisi hiyo.*




*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Regina Qwaray (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya Viongozi Chipukizi mara baada ya Naibu Waziri huyo kuzindua Programu ya Mafunzo kwa Viongozi hao Awamu ya Kwanza yaliofanyika jijini Dar es Salaam.*

# 6 FAHAMU KUHUSU GAZETI LA SERIKALI




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

*Fahamu kuhusu*

# GAZETI LA SERIKALI



MWAKA WA 106 — 12 Septemba, 2025

GAZETI LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TOLEO NA. 37 — DODOMA

Linatolewa kwa Idhini ya Serikali na Kuandikishwa Posta kama Gazeti

YALIYOMO

| Taarifa ya Kawaida | | Uk. |
|---|---|---|
| Notice re Supplements | Na. 12059 | 1/2 |
| Kupotea kwa Hati ya Kumiliki Ardhi | Na. 12078 | 2/6 |
| Kusajilowa kwa Hati | Na. 12079 | 6 |
| Kupotea kwa barua ya toleo | Na. 12080/1 | 6 |
| Kupotea Leseni ya Makazi | Na. 12082/4 | 6/7 |
| Kusudio la Kumilikisha Ardhi | Na. 12085 | 7 |
| Uteuzi wa Wajumbe wa Kamati ya Madalali na Wapeleka Wito wa Mabaraza ya Ardhi | Na. 12086 | 7 |
| Designation of Land | Na. 12087 | 7/8 |
| Mali Iliyopotea | Na. 12088/91 | 8 |
| Kampuni inayotarajiwa Kufutwa Kwenye Daftari la Makampuni | Na. 12092/120 | 8/12 |
| Winding Up | Na. 12121 | 12 |
| Final Meeting | Na. 12122 | 13 |
| Kufunga Kampuni | Na. 12123 | 13 |
| Business Registration | Na. 12124 | 13/4 |
| Uthibitisho wa Usimamizi wa Mirathi | Na. 12128/36 | 14/7 |
| Probate | Na. 12137/60 | 17/23 |
| Deed Poll | Na. 12161/392 | 23/113 |
| Affidavit | Na. 12393/4 | 113 |
| Kiapo | Na. 12395/6 | 113/4 |
| Inventory | Na. 12397/402 | 115/29 |
| Kusudio la Kuanzisha Hifadhi za Nyuki za Vijiji | Na. 12403 | 130/33 |

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 12059

Notice is hereby given that Regulation, Rules, Order, Notice, Kanuni, Amri and Notisi as Set out below, have been issued and are published in Subsidiary Legislation Supplement No. 36 dated 12th September, 2025 to this number of the Gazette:-

Regulation Under the Mining (Mineral Rights) (Amendment) (Government Notice No. 562 of 2025)

Regulation Under theMining (Local Content) (Amendment) (Government Notice No. 563 of 2025)

Regulation Under the Wildlife Conservation (Non-Consumptive Wildlife Utilization) (Amendment) (Government Notice No. 564 of 2025)

Order Under the Magistrates' Courts (Extension of Appellate Jurisdiction) (Revocation) (Government Notice No. 565 of 2025)

Order Under the Muhimbili University of Health and Allied Sciences (Establishment of Muhimbili University of Health and Allied Sciences Kigoma Campus College) (Government Notice No. 566 of 2025)

Order Under the Criminal Procedure (Extension of Jurisdiction) (Revocation) (Government Notice No. 567 of 2025)

Order Under the Muhimbili University of Health and Allied Sciences, (Establishment of Muhimbili University of

Matangazo yahusuyo mali za watu waliofariki, kuvunja mikataba ya ushirikiano na menginevyo, yakiwa ya manufaa kwa umma yaweza kuchapishwa katika Gazeti. Yapelekwe kwa **Mhariri, Ofisi ya Rais — Menejimenti ya Utumishi wa Umma, S. L. P. 670, 40404 Dodoma, Simu za Ofisi: +255(026)2963630.** Kabla ya Jumamosi ya kila Juma.

Limepigwa Chapa na Wakala wa Serikali wa Uchapishaji Tanzania - Dodoma

## Gazeti la Serikali ni nini?

Gazeti la Serikali ni kielelezo muhimu cha taarifa za Serikali, taasisi binafsi, wananchi na wadau mbalimbali zinazotumika katika utendaji wa kila siku.

## Gazeti la Serikali linamilikiwa na nani?

Gazeti la Serikali linamilikiwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

## Taarifa zinazotakiwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali kwa upande wa TAASISI ZA SERIKALI ni:-

- Mali isiyo na mwenyewe (Inventory)
- Maombi ya vibali vya maji
- Sheria ndogondogo za halmashauri
- Kanuni za kudumu za halmashauri mbalimbali
- Kutengwa kwa Ardhi kwa Madhumuni ya uwekezaji (Designation of land)
- Kampuni inayotajiriwa kufutwa
- Kampuni inayofutwa
- Uteuzi wa wajumbe wa baraza la ardhi
- Orodha ya wataalamu wa bodi
- Kusajili vyama vya wafanyakazi
- Matangazo ya serikali kuhusu masuala ya nchi
- Majina ya wakaguzi wa magari na wathamini madereva, n.k

*Itaendelea......*


ofisi_ya_rais_utumishi — www.utumishi.go.tz

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA**

*Fahamu kuhusu*

# GAZETI LA SERIKALI



MWAKA WA 106 — 12 Septemba, 2025

**GAZETI**

TOLEO NA. 37 — LA — DODOMA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

—O—

Linatolewa kwa Idhini ya Serikali na Kuandikishwa Posta kama Gazeti

YALIYOMO

| | Taarifa ya Kawaida | Uk. |
|---|---|---|
| Notice re Supplements | Na. 12059 | 1/2 |
| Kupotea kwa Hati ya Kumiliki Ardhi | Na. 12078 | 2/6 |
| Kusajilowa kwa Hati | Na. 12079 | 6 |
| Kupotea kwa barua ya toleo | Na. 12080/1 | 6 |
| Kupotea Leseni ya Makazi | Na. 12082/4 | 6/7 |
| Kusudio la Kumilikisha Ardhi | Na. 12085 | 7 |
| Uteuzi wa Wajumbe wa Kamati ya Madalali na Wapeleka Wito wa Mabaraza ya Ardhi | Na. 12086 | 7 |
| Designation of Land | Na. 12087 | 7/8 |
| Mali Iliyopotea | Na. 12088/91 | 8 |
| Kampuni inayotarajiwa Kufutwa Kwenye Daftari la Makampuni | Na. 12092/120 | 8/12 |
| Winding Up | Na. 12121 | 12 |
| Final Meeting | Na. 12122 | 13 |
| Kufunga Kampuni | Na. 12123 | 13 |
| Business Registration | Na. 12124 | 13/4 |
| Uthibitisho wa Usimamizi wa Mirathi | Na. 12128/36 | 14/7 |
| Probate | Na. 12137/60 | 17/23 |
| Deed Poll | Na. 12161/392 | 23/113 |
| Affidavit | Na. 12393/4 | 113 |
| Kupo | Na. 12395/6 | 113/4 |
| Inventory | Na. 12397/402 | 115/29 |
| Kusudio la Kuanzisha Hifadhi za Nyuki za Vijiji | Na. 12403 | 130/53 |

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 12059

Notice is hereby given that Regulation, Rules, Order, Notice, Kanuni, Amri and Notisi as Set out below, have been issued and are published in Subsidiary Legislation Supplement No. 36 dated 12th September, 2025 to this number of the Gazette:-

Regulation Under the Mining (Mineral Rights) (Amendment) (Government Notice No. 562 of 2025)

Regulation Under theMining (Local Content) (Amendment) (Government Notice No. 563 of 2025)

Regulation Under the Wildlife Conservation (Non-Consumptive Wildlife Utilization) (Amendment) (Government Notice No. 564 of 2025)

Order Under the Magistrates' Courts (Extension of Appellate Jurisdiction) (Revocation) (Government Notice No. 565 of 2025)

Order Under the Muhimbili University of Health and Allied Sciences (Establishment of Muhimbili University of Health and Allied Sciences Kigoma Campus College) (Government Notice No. 566 of 2025)

Order Under the Criminal Procedure (Extension of Jurisdiction) (Revocation) (Government Notice No. 567 of 2025)

Order Under the Muhimbili University of Health and Allied Sciences, (Establishment of Muhimbili University of

Matangazo yahusuyo mali za watu waliofariki, kuvunja mikataba ya ushirikiano na mengineyo, yakiwa ya manufaa kwa umma yaweza kuchapishwa katika Gazeti. Yapelekwe kwa **Mhariri, Ofisi ya Rais — Menejimenti ya Utumishi wa Umma, S. L. P. 670, 40404 Dodoma, Simu za Ofisi: +255(026)2963630.** Kabla ya Jumamosi ya kila Juma.

Limepigwa Chapa na Wakala wa Serikali wa Uchapishaji Tanzania - Dodoma

**Gazeti la Serikali ni nini?**

Gazeti la Serikali ni kielelezo muhimu cha taarifa za Serikali, taasisi binafsi, wananchi na wadau mbalimbali zinazotumika katika utendaji wa kila siku.

**Gazeti la Serikali linamilikiwa na nani?**

Gazeti la Serikali linamilikiwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

**Taarifa zinazotakiwa kuchapishwa katika Gazeti la Serikali kwa upande wa TAASISI NA WATU BINAFSI ni:-**

- Kubadili jina (Deed poll)
- Kufunga Kampuni
- Kupotea kwa hati ya kumiliki Ardhi
- Mali iliyopotea (Loss report)
- Mirathi
- Usimamizi Wa Mirathi
- Uthibitisho wa mirathi

*Itaendelea......*

ofisi_ya_rais_utumishi    www.utumishi.go.tz

# 7 SERIKALI YATOA VIBALI VYA AJIRA 86,500 KATIKA MWAKA WA FEDHA 2024/25 NA 2025/26

*Na Eric Amani - Dodoma*

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/25 na 2025/26, imetoa vibali vya ajira 86,500 ili kuhakikisha Wizara, Idara, Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinakuwa na watumishi wa kutosha kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi kikamilifu.

Akizungumza na Vyombo vya Habari Oktoba 11, 2025 jijini Dodoma, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Bw. Juma Mkomi amesema ajira hizo zinahusu kada mbalimbali ikiwemo Elimu, Afya, Kilimo, Uhandisi na sekta nyingine.

Katibu Mkuu Mkomi amefafanua kuwa katika mwaka wa fedha 2024/25 Serikali ilitoa kibali cha nafasi 45,000 za ajira mpya kwa Taasisi mbalimbali na utekelezaji wake ulianza tarehe 29 Aprili, 2025 na kufuatia kutolewa kwa kibali hicho, mchakato wa kujaza nafasi hizo umefanyika na hadi sasa nafasi 30,863 zimejazwa na wahusika wamepangiwa vituo vya kazi. Aidha, nafasi 6,701 usaili umefanyika na wahusika watapangwa vituo vya kazi ndani ya Mwezi Oktoba, 2025 na nafasi 7,436 ujazaji wake utakamilika Mwezi Novemba, 2025 na wasailiwa kupangwa vituo vya kazi mwezi huo huo.

Ameongeza kuwa katika mwaka wa fedha 2025/26, Serikali iliidhinisha nafasi 41,500 za ajira mpya kwa Taasisi mbalimbali zikiwemo nafasi 12,176 za Walimu na nafasi 10,280 za kada za Afya ambapo utekelezaji wake unaanza mara moja.

Kufuatia kutolewa kwa vibali hivyo, Katibu Mkuu Mkomi ameielekeza Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kuanza mchakato wa kujaza nafasi hizo za mwaka 2025/26 pamoja na kukamilisha mchakato wa nafasi zote za Mwaka 2024/25.

Vile vile Bw. Mkomi ametoa maelekezo kwa waajiri wote kutoa ushirikiano kwa Sekretarieti ya Ajira ili kuhakikisha lengo la ujazwaji wa nafasi za ajira linatimia.

“Ili kuhakikisha Sekretarieti ya Ajira inatekeleza jukumu hili ipasavyo, ninawaelekeza Waajiri kutoa ushirikiano. Aidha, ninawaelekeza Waajiri ambao Sekretarieti ya Ajira imekasimu madaraka ya uendeshaji wa mchakato wa ajira kwa baadhi ya kada, kuhakikisha wanaendesha usaili huu mara moja ili kujaza nafasi walizoidhinishiwa kwa kuzingatia Sheria, Taratibu na Kanuni za uendeshaji wa usaili katika Utumishi wa Umma,” Katibu Mkuu Mkomi amesisitiza.

Katika kuhakikisha gharama za kufanya usaili zinapungua na unafanyika kwa wakati, Bw. Mkomi ameielekeza Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kuwa zoezi la usaili lifanyike kila Mkoa Tanzania Bara na vituo vilivyoandaliwa mahsusi wa upande wa Zanzibar ili kutoa fursa kwa waombaji kutoka katika maeneo husika kuomba na hatimaye kusailiwa

Pia amesema waombaji watakaofaulu usaili lakini wakashindwa kupangiwa kazi baada ya usaili wawekwe katika kanzidata na waendelee kupangiwa kazi kwa kadri nafasi za ajira mpya zitakapokuwa zinapatikana.

Amesema waombaji hao watapangiwa kazi katika Taasisi zitakazokuwa na nafasi popote hapa nchini na kuongeza kuwa barua za kupangiwa vituo vya kazi kwa wasailiwa watakaofualu usaili zipatikane katika “Mfumo wa Ajira Portal” kupitia akaunti za wahusika.

Katibu Mkuu Mkomi ameongeza kuwa, Serikali itaendelea kutoa vibali vya ajira kulingana na mahitaji ya sekta mbalimbali ili kuhakikisha huduma bora kwa wananchi zinapatikana.



*Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Bw. Juma Mkomi akizungumza wakati wa Mkutano wake na Waandishi wa Habari kuhusu utoaji wa Vibali vya Ajira kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 na Mwaka 2025/26 uliofanyika katika Ofisi hiyo, Jijini Dodoma.*



*Sehemu ya Wakurugenzi wa Idara na Vitengo kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora wakimsikiliza Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Juma Mkomi (hayupo pichani) wakati wa Mkutano wake na Waandishi wa Habari kuhusu utoaji wa Vibali vya Ajira kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 na Mwaka 2025/26 uliofanyika katika Ofisi hiyo, Jijini Dodoma.*



*Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Bw. Juma Mkomi (meza kuu) akizungumza wakati wa Mkutano wake na Waandishi wa Habari kuhusu utoaji wa Vibali vya Ajira kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 na Mwaka 2025/26 uliofanyika katika Ofisi hiyo, Jijini Dodoma. Wengine ni Sehemu ya Wakurugenzi na Wakurugenzi Wasaidizi kutoka Ofisi hiyo.*

# 8 WATUMISHI WA UMMA WAKUMBUSHWA KUZINGATIA MAADILI KATIKA UTENDAJI KAZI ILI KUTOA HUDUMA BORA KWA WANANCHI



*Maafisa Sheria na Maafisa Utumishi wakifuatilia mada mbalimbali zilizokuwa zikitolewa na wawezeshaji (hawapo pichani) wakati wa kikao kazi kilicholenga kubadilishana uzoefu juu ya changamoto za utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma na kanuni zake mkoani Iringa*

*Na Antonia Mbwambo - Iringa*

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Regina Qwaray ametoa wito kwa Watumishi wa Umma nchini kuzingatia maadili ya utendaji katika utekelezaji wa majukumu yao ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mhe. Qwaray ameyasema hayo tarehe 27 Novemba, 2025 wakati akifungua kikao kazi kilichoshirikisha Maafisa Rasilimaliwatu na Maafisa Sheria kutoka taasisi za Serikali kwa lengo la kubadilishana uzoefu kuhusu ya changamoto mbalimbali zinazowakabili katika utekelezaji wa Sheria namba 298 ya Utumishi wa Umma na kanuni zake.

"Watumishi wa Umma mzingatie maadili na kufuata Kanuni, Taratibu na Miongozo iliyowekwa kwa mujibu wa Sheria ili kuondokana na changamoto katika utoaji wa huduma bila kujali unayemhudumia unamfahamu au haumfahamu kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi kwa manufaa ya Umma.

Aidha Mhe, Qwaray amesisitiza kwamba, kila Mtumishi wa Umma ana wajibu wa kuepusha migogoro na malalamiko mahali pa kazi lakini

pia kuutendea haki muda waliopewa na serikali katika kuhudumia wananchi.

Vilevile, Naibu Waziri Qwaray ametoa wito kwa watumishi wa Umma kutumia rasilimali zilizopo ipasavyo kwa kutekeleza majukumu yao kwa uaminifu na kwa wakati na kushirikiana katika kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi.

Awali, akitoa neno la utangulizi, Mkurugenzi wa Huduma za Sheria, Bi. Hilda Kabissa amesema kikao kazi hicho kimelenga kuchambua utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma ili kuimarisha utendaji kazi na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Kwa Upande wake, Mwakilishi wa Katibu Mkuu ambaye ni Mkurugenzi wa Usimamizi wa Maadili, Bi Felista Shuli wakati akimkaribisha Naibu Waziri kufungua kikao kazi hicho amesema kumekuwa na ukiukwaji wa Kanuni, Miongozo, Taratibu na Nyaraka mbalimbali zinazoandaliwa kwa ajili ya kuwapa mwongozo Watumishi wa Umma hivyo, kupitia kikao kazi hicho kitawezesha Watumishi kuwa na uelewa juu ya Sheria na Kanuni hizo kwa lengo la kuongeza uwajibikaji wenye tija.



*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Regina Qwaray akizungumza na Maafisa Sheria na Maafisa Utumishi wakati akifungua kikao kazi kilicholenga kuchambua Utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake ili kuimarisha utendaji kazi na kutoa huduma bora kwa wananchi.*



*Mkurugenzi wa Huduma za Sheria, Bi. Hilda Kabissa (aliyekaa katikati) akifuatilia hotuba ya mgeni rasmi ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Regina Qwaray wakati wa ufunguzi wa kikao kazi cha Maafisa utumishi na Maafisa Sheria kilichofanyika mkoani Iringa. Kulia kwake ni Mkurugenzi wa Usimamizi wa Maadili, Bi Felista Shuli na kushoto kwake ni Mkurugenzi wa Huduma za Sheria kutoka Tume ya Utumishi wa Umma, Bw. Charles Mulamula.*



*Naibu waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Regina Qwaray (aliyeshikanisha mikono) akiwasili kwa ajili ya ufunguzi wa kikao kazi cha maafisa Sheria na Maafisa Utumishi kilichofanyika katika Ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Iringa jijini Dodoma.*



*Maafisa Sheria na Maafisa Utumishi wakifuatilia mada mbalimbali zilizokuwa zikitolewa na wawezeshaji (hawapo pichani) wakati wa kikao kazi kilicholenga kubadilishana uzoefu juu ya changamoto za utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma na kanuni zake mkoani Iringa.*

# "IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA NI KIUNGO MUHIMU KATIKA HISTORIA YA NCHI YETU"- MHE. RIDHIWANI KIKWETE

*Na Antonia Mbwambo- Dodoma*

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete ametoa wito kwa Menejimenti na Watumishi wa Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa kuendelea kukusanya taarifa, kumbukumbu, nyaraka na machapisho mbalimbali yanayohusu historia ya nchi yetu na waasisi wa Taifa letu ili kutoa taswira ya nchi yetu kwa vizazi vijavyo.

Mhe. Kikwete ametoa wito huo akiwa kwenye mwendelezo wa ziara ya kikazi katika taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambapo leo ametembelea katika Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa jijini Dodoma.

"Niwapongeze kwa kazi nzuri mnayofanya ya kukusanya kumbukumbu na nyaraka, ninyi ni kiungo muhimu sana katika historia ya nchi yetu, tuna kazi kubwa ya kutunza kumbukumbu na kuweka nyaraka sawa. Historia ya Tanzania yetu iko chini ya Idara hii, jambo kubwa na la msingi ni kuhakikisha kazi hii inafanyika kwa ufanisi. Mimi na mwenzangu Naibu Waziri pamoja na watendaji wa Ofisi yetu tuko tayari kuwapa ushirikiano, ili tutekeleze vizuri majukumu yaliyoainishwa katika muundo wa taasisi hii," ameongeza Mhe. Kikwete.

Mhe. Kikwete pia ameielekeza Idara hiyo kuweka na kuhuisha mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu (Keyword filling system and e-file management system) katika Taasisi za Umma ili kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma Serikalini kwa kuwa suala hilo bado ni changamoto kubwa katika Taasisi nyingi za Umma.



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete (wa tatu kulia) akikabidhiwa Nyaraka za Ofisi na aliyekuwa Waziri wa Ofisi hiyo, Mh. Boniface Simbachawene (wa pili kulia) wakati wa makabidhiano ya ofisi yaliyofanyika tarehe 18 Novemba, 2025 Jijini Dodoma.*

Aidha, amewasisitiza kuendelea kutambua, kukusanya, kutunza na kuhifadhi kumbukumbu na vitu vya waasisi wa Taifa letu, kuendelea kuimarisha masijala katika Taasisi za Umma kwa kuzijengea uwezo Taasisi za Serikali kuhusu utunzaji wa kumbukumbu, kusimamia matumizi ya Mfumo wa e-Office na kuhakisha Roll Out ya Mfumo huo katika Taasisi zote za Umma pamoja na kusimamia maadili na taratibu za kiutendaji ili kukomesha vitendo vya uvujishaji wa Siri za Serikali;

Akitoa neno la utangulizi kabla ya kumkaribisha Mhe. Ridhiwani kuzungumza na watumishi wa Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Regina Qwaray ameipongeza Ofisi hiyo kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kutunza kumbukumbu na nyaraka za taifa.

“Nimejifunza mambo mengi, nimepata darasa la kutosha sikujua kama kuna mambo mengi hapa kabla ya sisi kuzaliwa,” Mhe. Qwaray ameongeza

Ametoa wito kwa Menejimenti na Watumishi wa Idara hiyo kutangaza utekelezaji wa majukumu ya taasisi yao ili watu wengi hasa vijana wa Tanzania wakajifunze na kujua historia ya nchi yao na kuwa wazalendo.



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete akisalimiana na Menejimenti na Watumishi wa Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa baada ya kuwasili katika Ofisi hiyo wakati wa ziara yake ya kikazi jijini Dodoma*



*Mkurugenzi Mkuu, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, Bw. Firimin Msiangi (wa kwanza kushoto) akifafanua jambo wakati Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete pamoja na Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, Mhe. Regina Qwaray walipokuwa wakielezwa namna historia ya Nchi na tamaduni mbalimbali za kitanzania zinavyotunzwa wakati wa ziara yao ya kikazi jijini Dodoma*



*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Regina Qwaray akieleza kwa Waziri wa Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Menejimenti na Watumishi wa Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa uzoefu wake kwa baadhi ya tamaduni za sehemu ya makabila wakati wa ziara yao ya kikazi katika ofisi hiyo jijini Dodoma.*

# 10 MATUKIO KATIKA PICHA YAKIONYESHA USHIRIKI WA OFISI YA RAIS-UTUMISHI NA UTAWALA BORA KATIKA WIKI YA HUDUMA KWA MTEJA KUANZIA TAREHE 6-10 OKTOBA, 2025 ILIYOKUWA NA KAULIMBIU ISEMAYO DHAMIRA INAYOWEZEKANA










*Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Juma Mkomi akizingumza na Viongozi na Watumishi wa ofisi yake suala la kutunza amani wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo yanayofanyika kila Jumatatu kwa watumishi hao katika Ofisi zilizopo Mtumba jijini.*

# 11 KATIBU MKUU MKOMI AWASISITIZA WATUMISHI WA UMMA KUDUMISHA AMANI

*Na Mwandishi Wetu - Dodoma*

Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Bw. Juma Mkomi, ametoa wito kwa Watumishi wa Umma nchini kuendelea kudumisha amani, mshikamano na uzalendo katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku kwa manufaa ya Taifa.

Akizungumza jijini Dodoma wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi wa ofisi hiyo yanayofanyika kila siku ya Jumatatu, Katibu Mkuu Mkomi amesema, Utumishi wa Umma una nafasi kubwa katika kulinda na kuimarisha amani ya nchi kwa kutoa huduma bora, kuzingatia maadili ya kazi na kuepuka vitendo vinavyoweza kuleta mgawanyiko katika jamii.

"Watumishi wa Umma ni kioo cha Serikali, hivyo mnapaswa kuwa mfano katika uadilifu, uvumilivu na uzalendo," alisema Katibu Mkuu Mkomi.

Bw. Mkomi pia aliwakumbusha watumishi kuzingatia misingi ya utawala bora, uwajibikaji, na matumizi sahihi ya rasilimali za umma, sambamba na kutumia lugha na mienendo inayojenga taswira chanya ya Serikali.

Kwa upande wake mwewezeshaji ambaye ni Mkurugenzi wa Kitengo cha Ulinzi na Usalama wa TEHEMA, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Bw. Mussa Chiwelenje amewasisitiza Watumishi kutunza taarifa zao binafsi, za Ofisi na kutochezea miundombinu ya TEHAMA kwa usalama wa Taifa.



*Sehemu ya Watumishi wa Ofisi ya Rais-UTUMISHI wakimsikiliza Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Juma Mkomi (hayupo pichani) wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo yanayofanyika katika ofisi hiyo iliyopo Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma.*



*Sehemu ya Watumishi wa Ofisi ya Rais-UTUMISHI wakimsikiliza Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Juma Mkomi (hayupo pichani) wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo yanayofanyika katika ofisi hiyo iliyopo Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma.*



*Sehemu ya Wakurugenzi wa Ofisi ya Rais-UTUMISHI, wakimsikiliza Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Juma Mkomi (hayupo pichani) wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo yanayofanyika katika ofisi hiyo iliyopo Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma.*

# 12 WITO WATOLEWA KWA WATUMISHI WA UMMA KUBADILIKA KIMTAZAMO KATIKA UTENDAJI ILI KUFIKIA MALENGO YA DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2050

*Na Antonia Mbwambo - Dodoma*

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Xavier Daudi ametoa wito kwa Watumishi wa Umma nchini kubadilika kimtazamo katika utendaji ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ikiwemo matumizi sahihi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Bw. Daudi ametoa wito huo tarehe 13 Novemba, 2025 alipokuwa akizungumza na watumishi wa Ofisi hiyo eneo maalum linalotumika kutoa mafunzo katika Ofisi hiyo Mtumba jijini Dodoma, yanayofanyika kila siku ya Jumatatu kwa lengo la kuwajengea uwezo watumishi hao ili kuboresha Utendaji kazi.

Naibu Katibu Mkuu Bw. Daudi amesema, Watumishi wa Umma kubadilika kimtazamo katika utendaji ni jambo muhimu kwani kunakuwa na ufanisi wa kazi unaowezesha kuwa na Taifa jumuishi lenye ustawi, haki na linalojitegemea.

"Ninatoa wito kwenu, msitekeleze majukumu yenu kwa mazoea, kupitia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, mbadilike kiutendaji ili kuendana na mabadiliko yakiwemo ya kidijiti kwa kuleta ubunifu na mawazo chanya yatakayoiwezesha serikali kufikia malengo yake ya kutoa huduma bora kwa wananchi kupitia matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA," Bw. Daudi alisema.

Kwa upande wake Meneja Mawasiliano Serikalini kutoka Tume ya Taifa ya Mipango (NPC), Bw. Titus Kaguo wakati akiwasilisha mada kwa watumishi hao kuhusu Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, amesema mabadiliko makubwa ya Sayansi na Teknolojia ni kichocheo kikubwa cha maendeleo katika Taifa letu ambapo Dira hii imelenga kuwa kufikia mwaka 2050, asilimia 70 ya Watanzania watakuwa wanatumia mifumo ya TEHAMA na asilimia 80 ya huduma mbalimbali za kiserikali zitakuwa zikitolewa kidiji ili kuleta Ufanisi katika Utendaji.



*Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Xavier Daudi (aliyesimama mbele) akizungumza na watumishi wa Ofisi hiyo baada ya wasilisho la mada ya Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 lililotolewa na Meneja Mawasiliano Serikalini kutoka Tume ya Taifa ya Mipango (NPC), Bw. Titus Kaguo (hayupo pichani) katika mafunzo ya kuwajengea watumishi wa Ofisi hiyo uwezo wa kiutendaji jijini Dodoma.*



*Wakurugenzi wa Idara na vitengo mbalimbali kutoka Ofisi ya Rais-UTUMISHI wakimsikiliza Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Xavier Daudi alipokuwa akisisitiza jambo kuhusu Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 mara baada ya kupatiwa mafunzo ambayo hutolewa kila siku ya jumatatu kwenye Ofisi hiyo iliyopo Mtumba jijini Dodoma.*



*Sehemu ya Watumishi wa Ofisi ya Rais-UTUMISHI wakimsikiliza Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI Bw. Xavier Daudi (hayupo pichani) wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo yanayofanyika katika ofisi hiyo iliyopo Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma.*



*Wakurugenzi wa Idara na vitengo mbalimbali kutoka Ofisi ya Rais-UTUMISHI wakimsikiliza Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Xavier Daudi (hayupo pichani) wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo yanayofanyika katika ofisi hiyo iliyopo Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma.*

# 13 MRADI WA UJENZI WA MAKAZI YA WATUMISHI WA UMMA SEKTA YA ELIMU NA AFYA KUONGEZA TIJA KATIKA UTENDAJI KAZI



*Kaimu Mkurugenzi wa Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini, Ofisi ya Rais-UTUMISHI na Utawala Bora, Bw. Patrick Allute (aliyenyanyua mkono) akizungumza jambo wakati Timu ya wataalam kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wizara ya Fedha na Watumishi Housing Investments ikikagua na kufanya tathmini ya mwisho ya kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa makazi ya Watumishi wa Umma katika Kijiji cha Makunda, Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, mkoani Singida. Wengine ni Watumishi wa Zahanati ya Makunda.*

*Na Veronica Mwafisi*

imu ya wataalam kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wizara ya Fedha na Watumishi Housing Investments ikiongozwa na Kaimu Mkurugenzi wa Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini, Ofisi ya Rais-UTUMISHI na Utawala Bora, Bw. Patrick Allute imefanya ziara ya kikazi iliyolenga kukagua na kufanya tathmini ya mwisho ya kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa makazi ya Watumishi wa Umma katika mikoa ya Dodoma, Singida, Lindi, Pwani na Ruvuma unatarajiwa kuongeza ufanisi na uwajibikaji kwa watumishi wa umma Serikalini.

Akizungumza kwa niaba ya timu hiyo mara baada ya kukagua miradi hiyo, Kaimu Mkurugenzi Allute amesema, makazi ya watumishi wa umma yanapokuwa karibu na maeneo ya kazi huongeza ufanisi na uwajibikaji hivyo, utekelezaji wa mradi huo kwa awamu ya kwanza katika mikoa hiyo utamkomboa mtumishi wa umma katika utendaji kazi.

"Maeneo ya pembezoni yamekuwa na changamoto ya makazi na kusababisha baadhi ya watumishi wa umma kutokutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, hivyo kupitia mradi huu unaotekelezwa kwa awamu ya kwanza tunaamini uwajibikaji kwa watumishi wa umma kwenye maeneo hayo utaongezeka," amesema Mkurugenzi Allute.

Naye, Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Mipango na Bajeti, Bi. Julieth Magambo amesema ili makazi hayo yawe na ubora wa kudumu ni vema Watumishi watakaoishi katika makazi hayo wakazingatia utunzaji wa miundombinu.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Fedha na Uwekezaji kutoka Watumishi Housing Investments, Bw. Paskali Massawe, amesema makazi hayo yamejengwa kwa kuzingatia ubora ili kuendana na malengo ya Serikali katika kuwatengenezea mazingira bora watumishi wa umma.



*Mwonekano wa jengo la mradi wa makazi ya Watumishi wa Umma lililopo katika Kijiji cha Kijiweni, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi mkoani Lindi.*

*Mwonekano wa jengo la mradi wa makazi ya watumishi wa umma lililopo katika Kituo cha Afya Kilagano, Halmashauri ya Wilaya ya Songea, mkoani Ruvuma.*





*Mwonekano wa jengo la mradi wa makazi ya watumishi wa umma lililopo katika Kituo cha Afya Kilagano, Halmashauri ya Wilaya ya Songea, mkoani Ruvuma.*

*Mwonekano wa jengo la mradi wa makazi ya Watumishi wa Umma lililopo katika Zahanati ya Makunda, Kijiji cha Makunda, Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, mkoani Singida.*





# 14 TUJIKITE KUFUNDISHA KOZI ZITAKAZOENDA KUTATUA CHANGAMOTO ZA WAHITIMU NA WANANCHI - MHE. KIKWETE

*Na Eric Amani - Dar es Salaam*

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete ameielekeza Bodi ya Ushauri na Menejimenti ya Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC) kujikita zaidi katika kufundisha kozi zitakazoenda kutatua changamoto za wahitimu na wananchi kwa ujumla.

Waziri Kikwete ametoa maelekezo hayo tarehe 28 Novemba, 2025 kabla ya kuwatunuku wahitimu wa kozi mbalimbali katika mahafali ya 42 ya Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania yaliyofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam.

Mhe. Kikwete amesema, Watanzania wanahitaji kupata elimu ya kuwasaidia katika maisha yao na sio ya kukaa na vyeti ndani. "Naielekeza Bodi na Menejimenti kuhakikisha Kozi tunazoanzisha zinaleta majawabu ya changamoto za Watanzania," Mhe. Kikwete amesisitiza.

Mhe. Kikwete amesema anayo maswali ya msingi ya kujiuliza, akitolea mfano wa Kozi ya Makatibu Mahususi, je Kozi zilizotolewa kwa watumishi hawa zamani zinafanana na zinazotolewa sasa? Tumeshuhudia uvunjifu wa maadili kwa watumishi. Ni wajibu wetu kuhakikisha watumishi wanakuwa na uadilifu, tutengeneze Utumishi wa Umma wenye weledi. Je watumishi wa umma bado ni wazalendo? Ni majibu yanayopatikana kwa Menejimenti na Bodi ya Chuo hiki. Tuangalie Mitaala ili ijibu maswali yangu," amesisitiza.

Mhe. Kikwete amesema, Watanzania wanahitaji kupata elimu ya kuwasaidia katika maisha yao na sio ya kukaa na vyeti ndani. “Naielekeza Bodi na Menejimenti kuhakikisha Kozi tunazoanzisha zinaleta majawabu ya changamoto za Watanzania,” Mhe. Kikwete amesisitiza.

Mhe. Kikwete amesema anayo maswali ya msingi ya kujiuliza, akitolea mfano wa Kozi ya Makatibu Mahususi, je Kozi zilizotolewa kwa watumishi hawa zamani zinafanana na zinazotolewa sasa? Tumeshuhudia uvunjifu wa maadili kwa watumishi. Ni wajibu wetu kuhakikisha watumishi wanakuwa na uadilifu, tutengeneze Utumishi wa Umma wenye weledi. Je watumishi wa umma bado ni wazalendo? Ni majibu yanayopatikana kwa Menejimenti na Bodi ya Chuo hiki. Tuangalie Mitaala ili ijibu maswali yangu,” amesisitiza.



Akiwasilisha hotuba ya Katibu Mkuu-UTUMISHI kabla ya kumkaribisha Waziri Kikwete kuzungumza na wahitimu hao, Mwakilishi wa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Nolasco Kipanda amewapongeza wadau wote waliofanikisha Chuo hiki kuendelea na kuwapongeza pia wahitimu kwa kutunukiwa vyeti na kuwasisitiza kuitumia vyema elimu waliyoipata.

Amesema Serikali imeendelea kukijengea uwezo Chuo cha Utumishi wa Umma kupitia miradi ya kimkakati yenye tija.

Akiwasilisha taarifa ya utendaji wa Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC) Mtendaji Mkuu na Mkuu wa TPSC, Dkt. Ernest Mabonesho amesema jumla ya wahitimu 6956 kutoka katika kampasi zote sita za TPSC ambazo ni Dar es Salaam, Tanga, Mtwara, Tabora, Singida na Mbeya wametunukiwa vyeti katika ngazi ya shahada, stashahada na astashahada katika kozi mbalimbali.



## 15 MHE. RIDHIWANI KIKWETE AITAKA SEKRETARIETI YA AJIRA KUHARAKISHA NA KUWEKA WAZI MCHAKATO WA AJIRA 12,000 ZILIZOTANGAZWA NA RAIS MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN

*Na Antonia Mbwambo - Dodoma*

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete ameitaka Menejimenti ya Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kuharakisha na kuweka wazi mchakato wa ajira 12,000 zilizotangazwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati akifungua rasmi Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 14 Novemba, 2025 jijini Dodoma.

Mhe. Kikwete ameyasema hayo tarehe 24 Novemba, 2025 ikiwa ni ziara yake ya kwanza katika taasisi hiyo tangu alipoapishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 18 Novemba, 2025 kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Amesema moja ya ahadi za Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha Utumishi wa Umma unakuwa bora katika kutekeleza majukumu ya utoaji wa huduma bora kwa wananchi na kuongeza kuwa ili kuhakikisha hili linaanza kutekelezwa aliahidi kutoa vibali vya ajira 12,000 kwa Kada ya Elimu watumishi 7,000 na Kada ya Afya, watumishi 5,000.

"Kibali cha ajira kimeshatolewa, nawashukuru kwa kuanza kufanyia kazi, ni jambo zuri, ni mategemeo yangu kuwa majawabu ya maelekezo ya Mhe. Rais tutayaona hivi karibuni, hakikisheni mnasimamia kwa ukamilifu, mchakato wote wa ajira hizi uwekwe wazi ili kuondoa dhana potofu ya kuwa kuna upendeleo katika kutoa ajira." Mhe. Kikwete amesisitiza.

Ameitaka Menejimenti hiyo kuongeza kasi ya kuratibu mchakato wa ajira "Tuangalie changamoto zinazokwamisha uharakishaji wa mchakato wa ajira ili tuweze kutatua na kuendelea na kukamilisha kwa wakati." Ameongeza.

Aidha, ameisisitiza Menejimenti hiyo kutoonea watumishi walio chini yao bali wawaelekeze kwa upendo. "Tusimamie maadili katika utekelezaji wa majukumu yetu, tusionee watumishi walio chini yetu, tuzingatie taratibu za utendaji kazi." Ameongeza

Pamoja na maelekezo aliyoyatoa kwa Menejimenti hiyo, Mhe. Kikwete ameomba ushirikiano katika utekelekezaji wa majukumu ya Serikali ili kufikia malengo ya Serikali ya utoaji wa huduma bora kwa ustawi wa taifa

Amewapongeza kwa kutekeleza maelekezo ya Wabunge katika kuendesha usaili ngazi ya mkoa na wanaopangiwa kazi kupokelea barua za ajira katika mikoa yao.

"Nawashukuru, pamoja na kuwa nilikuwa katika Ofisi nyingine lakini mmefanya kazi nzuri, tuendelee tusirudi nyuma, suala la kufanya mahojiano mikoani na kuchukua barua za ajira mikoani limeweza kupunguza kadhia." Amesema.

Katika hatua nyingine, amewapongeza kwa kuanzisha Kituo cha Huduma kwa Mteja (call centre) kwani itapunguza adha kwa wenye uhitaji wa huduma na kuwasisitiza kuwaweka watumishi wenye kauli nzuri.

Naye Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Regina Qwaray amesisitiza ushirikiano toka kwa Menejimenti hiyo. "Tumekuja kujitambulisha, ninaomba ushirikiano wenu, tufanye kazi kwa pamoja, tutatue kero za wananchi kama ambayo Rais wetu anatamani iwe.

Aidha amepongeza kazi inayofanyika katika taasisi hiyo. "Ni mara yangu ya kwanza kufika katika jengo hili, ni masaa machache nimetembelea katika jengo hili lakini napenda niwapongeze nimeona kazi zinavyofanyika, hongereni sana.

Kwa upande wake, Katibu wa Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma, Bwana Mick Kiliba akielezea majukumu ya Taasisi hiyo, amemshukuru Mhe. Waziri na Viongozi wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora aliombatana nao kwa kuona umuhimu wa kutembelea katika Ofisi hiyo na kuwahimiza uwajibikaji kwa maslahi mapana ya taifa.

Akiainisha mafanikio mbalimbali ya Taasisi hiyo, Bw. Kiliba amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwawezesha kumiliki jengo lao ambapo sasa watumishi wote wako katika jengo moja na kuwaongezea bajeti ya utekelezaji wa majukumu yao ya masuala ya ajira.



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete akizungumza na Menejimenti ya Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (hawapo pichani) wakati wa ziara yake ya kikazi katika Ofisi hiyo tarehe 24 Novemba, 2025 jijini Dodoma*



*Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Bw. Juma Mkomi akizungumza jambo kuhusu utendaji kazi wa kituo cha Huduma kwa Mteja wakati wa ziara ya kikazi ya Waziri wa Ofisi hiyo Mhe. Ridhiwani Kikwete (kulia kwake) na Naibu Waziri wa Ofisi hiyo Mhe. Regina Qwaray (kushoto kwake) walipofanya ziara ya kikazi Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma jijini Dodoma.*



*Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Bw. Innocent Bomani (aliyenyoosha mkono) akitoa maelezo mafupi kuhusiana na utendaji kazi wa kituo cha Huduma kwa Mteja wakati wa ziara ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete katika Ofisi hiyo jijini Dodoma.*



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete (wa tatu kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Menejimenti ya Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma wakati wa ziara yake ya kikazi katika Ofisi hiyo jijini Dodoma. kulia kwake ni Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Regina Qwaray na Kushoto kwake ni Katibu wa Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma, Bw. Mick Kiliba.*

# HABARI KATIKA PICHA



*Mwenyekiti wa UTUMISHI Saccos ambaye ni Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Utawala, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bi. Nyasinde Mukono akizungumza na Wanachama wa Saccos hiyo wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka 2025 uliofanyika katika ofisi hiyo iliyopo Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma.*



*Sehemu ya Wakurugenzi wa Ofisi ya Rais-UTUMISHI ambao pia ni Wanachama wa UTUMISHI Saccos wakimsikiliza Mwenyekiti wa UTUMISHI Saccos ambaye ni Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Utawala, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bi. Nyasinde Mukono (hayupo pichani) wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka 2025 uliofanyika katika ofisi hiyo iliyopo Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma.*



*Sehemu ya Wakurugenzi wa Ofisi ya Rais-UTUMISHI ambao pia ni Wanachama wa UTUMISHI Saccos wakimsikiliza Mwenyekiti wa UTUMISHI Saccos ambaye ni Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Utawala, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bi. Nyasinde Mukono (hayupo pichani) wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka 2025 uliofanyika katika ofisi hiyo iliyopo Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma.*




*Mwenyekiti wa UTUMISHI Saccos ambaye ni Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Utawala, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bi. Nyasinde Mukono (watatu kutoka kushoto mbele) akiwa katika picha ya pamoja na Sehemu ya Wakurugenzi na Watumishi wa ofisi hiyo ambao ni Wanachama wa UTUMISHI Saccos mara baada ya kuhitimisha Mkutano Mkuu wa Mwaka 2025 uliofanyika katika ofisi hiyo iliyopo Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma.*



*Sehemu ya Wakurugenzi na Watumishi wa Ofisi ya Rais-UTUMISHI ambao pia ni Wanachama wa UTUMISHI Saccos wakimsikiliza Mwenyekiti wa UTUMISHI Saccos ambaye ni Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Utawala, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bi. Nyasinde Mukono (hayupo pichani) wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka 2025 uliofanyika katika ofisi hiyo iliyopo Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma.*

**IMETOLEWA NA**

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi
wa Umma na Utawala Bora

Desemba, 2025